# Kuzuia marufuku adhabu zote za viboko kwa watoto

## Majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara



Pia kwenye msururu huu:

**Kupiga marufuku adhabu zote za viboko kwa watoto:
Maswali na majibu kwa vijana na watoto**

**Kuzuia adhabu ya viboko shuleni:
Majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara**

KIMECHAPISHWA 2009 NA:

**Mpango wa Kimataifa wa Kukomesha Adhabu zote za Viboko kwa Watoto**

KIMECHAPISHWA 2017 NA:

**Mpango wa Kimataifa wa Kukomesha Adhabu zote za Viboko kwa Watoto** (Global Initiative to End All Corporal Punishment of Children)

www.endcorporalpunishment.org

Mpango wa Kimataifa wa Kukomesha Adhabu zote za Viboko kwa Watoto umesajiliwa Uingereza na Wales kama kampuni ndogo nambari 2354395 na ya hisani nambari 328132.

Ofisi iliyosajiliwa: The Foundry, 17 Oval Way, London SE11 5RR, UK.


**Shirika la Save the Children Sweden**

www.raddabarnen.se; resourcecentre.savethechildren.net

Save the Children Sweden ni sehemu ya Chama cha Save the Children, Shirika la Misaada lenye mashirika 29 tofauti ya Save the children, kilichosajiliwa Uswizi na ni moja ya mashirika makubwa duniani ya Haki za Watoto. Shirika la Save the Children pia ni mmiliki wa Save the Children International (SCI), ambalo ni shirika linalotekeleza mpango wa kimataifa.

Makao Makuu ya Ofisi za Save the Children Sweden: Radda Barnen, SE-107 88 Stockholm, Landsvagen 39, Sundyberg, Sweden.

Wakati tukifikiria kuzuia adhabu zote za viboko kwa watoto maswali mengi yanajitokeza, hasa kuhusiana na kile ambacho katazo litamaanisha kwa wazazi na maisha ya familia. Kitabu hiki kinatoa majibu ya maswali yanayoulizwa mara nyingi na kukanusha fikra potofu zilizojengeka juu ya sababu za kuzuia na athari zake kwa familia.



# Maswali

**Sehemu ya 1: Maswali kuhusu sababu za kuzuia adhabu zote za viboko**


**8** Je, adhabu ya viboko huumiza?

**10** Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto ni nini, na mkataba huo unasema nini kuhusu adhabu ya viboko kwa watoto?

**12** Kura za maoni zinasema kwamba watu wengi wanapinga kupiga marufuku rasmi adhabu ya viboko. Je, hatupaswi kuwasikiliza watu?

**13** Mara nyingi nimewasikia vijana wakiongelea kuunga mkono adhabu ya viboko – kwa kweli tunapaswa kuwasikiliza wao?

**14** Kupigwa kama mtoto hakuwa na madhara yoyote. Ningekuwa hapa nilipo leo ikiwa wazazi wangu wasingeniadhibu kwa viboko?

**17** Kuna ukiukwaji mwingi mbaya sana wa haki za watoto – kwa nini tujikite kwenye suala dogo hili?

**18** Wazazi wana haki ya kuwalea watoto wao kama wanavyoona inafaa. Je, hawapaswi kupingwa tu katika hali mbaya za unyanyasaji wa watoto?

**20** Kuna tofauti kubwa kati ya kumpiga mtoto na kumchapa bila kumuumiza. Je, kuzuia adhabu ya viboko siyo kuchukua hatua ya mbali mno?

**23** Kwa nini tusielezee kuchapa bila kuumiza, badala ya kuzuia adhabu hiyo yote?

**24** Dini yangu inanihitaji kutumia adhabu ya viboko. Je, haitakuwa ubaguzi kunikataza kutumia adhabu hiyo?

**26** Kwa nini tulete sheria katika swala hili? Kwa nini wazazi wasielimishwe tu kuacha kutumia adhabu ya viboko?

**27** Wakati mwingi adhabu ya viboko hufanyika katika familia nyuma ya milango iliyofungwa; itakuwa vigumu kupiga marufuku, hivyo nini maana ya kuizuia?

**28** Hatupaswi kusubiri hadi hali ya kila siku iimarike kwa wazazi na waalimu kabla ya kuzuia adhabu ya viboko, ili isiongeze tu mfadhaiko wao?

**31** Hili ni suala muhimu, linalozingatiwa katika Bara la Ulaya. Adhabu ya viboko ni sehemu ya utamaduni wangu na mazoea ya malezi ya watoto. Je, si ubaguzi kupiga marufuku sheria hii?

**32** Kwa nini ni vigumu sana kuacha kupiga watoto?

**Sehemu ya 2: Maswali kuhusu athari ya kuzuia adhabu zote za viboko**

**36** Ikiwa wazazi wakilazimishwa kuacha adhabu ya viboko, je watoto hawataishia kuharibika na kukosa nidhamu?

**39** Kama adhabu ya viboko ikipigwa marufuku, si kwamba itasababisha watoto kuadabishwa kwa njia nyingine za kutisha zaidi – unyanyasaji wa kihisia, udhalilishaji au kuwafungia ndani?

**40** Kama adhabu ya viboko ni kosa la jinai, si maelfu ya wazazi watashtakiwa na watoto wengi kupelekwa gerezani?

**42** Je, si sawa kwa wazazi kuwachapa watoto wao kuwazuia kuumizana wenyewe?

# Sehemu ya 1: Maswali kuhusu sababu za kuzuia adhabu zote za viboko



# Je, adhabu ya viboko kweli huumiza?

Ndiyo, bila shaka huumiza! Ni chungu kimwili na kihisia. Kupitia utafiti unaofanywa duniani kote, watoto wanaanza kutuambia ni kiasi gani adhabu ya viboko inawaumiza. Utafiti wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa juu ya Unyanyasaji wa Watoto, uliokamilika mwaka 2006, ulikuwa utafiti wa kwanza mpana wa kimataifa kuhusu chanzo na kiwango cha tatizo. Mtaalamu wa kujitegemea aliyeongoza utafiti huu, Profesa Paulo Sergio Pinheiro, aliandika katika ripoti hiyo:[1]

"Katika mchakato mzima wa utafiti huo, watoto wamekuwa kila mara wakielezea haja ya dharura ya kuzuia unyanyasaji huu wote". Watoto wanashuhudia madhara – si tu ya kimwili, lakini 'madhara ndani' – ambayo unyanyasaji huu husababisha, ikichangiwa na kukubalika na watu wazima, hata kuuidhinisha.

Serikali zinahitaji kukubali kwamba hili kweli ni jambo la dharura, ingawa sio dharura mpya. Watoto wameteseka na unyanyasaji mikononi mwa watu wazima bila kuonekana na kusikika kwa karne nyingi. Lakini sasa kwamba kiwango na athari za unyanyasaji wa watoto zinakuwa wazi, hawawezi kuachwa kusubiri zaidi kwa ajili ya kupewa ulinzi wa ufanisi ambao hawana haki nao." Je, adhabu ya viboko kweli huumiza?

Kusababisha maumivu ya kimwili kwa mtoto yenyewe ni uvunjaji wa haki ya watoto ya kulindwa kutokana na shambulio – na watu wazima mara nyingi hawatambui tofauti za ukubwa na nguvu kati yao na mtoto, na

1. Pinheiro, P. S. (2006), Ripoti ya Ulimwengu kuhusu vurugu dhidi ya watoto, Geneva: Uchunguzi ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Vurugu dhidi ya watoto. Kwa taarifa zaidi kuhusu Uchunguzi na kupakua ripoti, tazama: www.ohchr.org/EN/HRBodies/CRC/Study/Pages/StudyViolenceChildren.aspx.

athari ambayo tofauti hii inaweza kuleta kwa walengwa na maumivu halisi ya kimwili anayohisi mtoto. Utafiti mkubwa uliofanyika ambapo wazazi waliulizwa kuhusu nguvu iliyotumika wakati wakimchapa mtoto wao uligundua kwamba wazazi wawili kati ya watano walitumia kiwango cha nguvu tofauti kuliko walivyonuia.[2] Na utafiti uliofanywa na Taasisi ya Tiba ya Akili na Chuo cha London umebainisha kwamba mabadiliko katika kazi ya ubongo wakati nguvu ikitumika katika hali ya kulipiza kisasi kawaida husababisha kuongezeka kwa kiwango cha nguvu kutumika na kutokuwa na usahihi katika kuhukumu nguvu kiasi gani inatumika.[3]

Aidha, watu wazima mara nyingi hawafahamu madhara ya kihisia yanayosababishwa na adhabu ya viboko, athari zake kwa heshima ya mtoto, na uwezekano wa madhara ya muda mfupi na ya muda mrefu kwa watu binafsi na jamii. Mpango wa Kimataifa unazitambua tafiti zaidi ya 250 juu ya athari ya adhabu ya viboko ambayo huhusisha matatizo mbalimbali ya kiafya, athari za kiukuaji na kitabia kwa watoto ambazo huweza kuwafuata hadi ukubwani- hii ni pamoja na afya duni ya akili, uwezo mdogo katika masomo, ufaulu wa chini shuleni, kuongezeka magomvi, kanuni duni za maadili na kuongeza kwa tabia zisizoendana na jamii.[4]

2. Kirwaun, S. & Bassett, C. (2008), Uwasilishaji kwa NSPCC: Adhabu ya viboko, Ofisi ya Utafiti wa Masoko Uingereza/Jumuiya ya Taifa ya Kuzuia Ukatili kwa Watoto.

3. Shergill, S. S. et al (2003), “Two eyes for an eye: The neuroscience of force escalation”, Science, vol. 301, 11 July 2003, p. 187.

4. Kwa taarifa zaidi, tazama: Adhabu ya kichapo kwa watoto: Muhtasari wa utafiti kuhusu matokeo na mahusiano yake, kwenye: endcorporalpunishment.org/resources/research.

# Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto ni nini, na unasema nini kuhusu adhabu ya viboko?

Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto ni nini, na unasema nini kuhusu adhabu ya viboko?

Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto, au UNCRC, ni tamko kamili zaidi kuhusu haki za watoto lililowahi kuandikwa na ni azimio kubwa zaidi lililopata kuridhiwa kimataifa katika historia. Mkataba una vifungu 54 vinavyohusisha nyanja zote za maisha ya mtoto na kuweka haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni ambazo zinawahusu watoto wote kila mahali.

Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Mtoto ina jukumu la kuhakikisha Mkataba unazingatiwa vizuri na nchi zilizosaini na kuutekeleza. Kamati imeweka wazi kwamba Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Mtoto (UNCRC) inahitaji kuzuia sheria na vitendo vyote vya adhabu kali katika mazingira yote – nyumbani, mazingira ya huduma mbadala, vituo vya chekechea, shuleni na mifumo mingine ya adhabu. Maoni ya Jumla ya Kamati Namba 8 (2006) kuhusu "Haki ya mtoto dhidi ya adhabu ya viboko na aina nyingine za adhabu za ukatili au za kudhalilisha (sanaa. 19; 28, aya. 2; na 37, pamoja na)" iliimarisha na kuthibitisha majukumu haya, yaliyotajwa katika Maoni ya Jumla nambari 13 (2011) kuhusu "Haki ya mtoto juu ya uhuru dhidi ya aina zote za vurugu ".

Mara kwa mara kamati inachunguza jinsi nchi zinavyotekeleza Haki za Mtoto na huwa inapendekeza utaratibu wa kuzuia adhabu ya viboko inapofikia uchunguzi wake wa mwisho. Mipango mingine ya ufuatiliaji wa mkataba pia inapendekeza upigaji marufuku na suala hili linaibuliwa mara kwa mara katika mapitio ya Mara kwa Mara ya Kidunia (Universal Periodic Review) kuhusu rekodi za haki za binadamu kwa ujumla.

# Kura nyingi za maoni zinasema kwamba watu wengi wanapinga amri rasmi ya kupiga marufuku adhabu ya viboko. Je, hatupaswi kuwasikiliza watu?

Kura nyingi za maoni zinasema kwamba watu wengi wanapinga amri rasmi ya kupiga marufuku adhabu ya viboko. Je, hatupaswi kuwasikiliza watu?

Katika suala hili – kama mengineyo, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji dhidi ya wanawake na ubaguzi wa rangi – wanasiasa wanapaswa kuongoza, sio kufuata maoni ya umma. Msisitizo uwe kwenye wajibu wa serikali kuhakikisha kwamba sheria inawapa watoto ulinzi wa kutosha kwa utu wao wa kibinadamu kama ilivyo kwa watu wazima.

Karibu nchi zote ambazo zimezuia adhabu zote za viboko, zimefanya hivyo bila kujali maoni ya umma, na baadae maoni ya umma yakaja kwa haraka kuunga mkono mabadiliko. Baada ya miaka kadhaa tutaangalia tulikotoka kwa mshangao – na kwa aibu – kipindi ambacho ilichukuliwa kuwa ni ya kisheria and inakubalika kuwapiga watoto.

Matokeo ya kura ya maoni hutegemea jinsi maswali yalivyoundwa na kama wanaopiga kura ya maoni wana taarifa za kutosha. Ikiwa watu wana taarifa za kutosha kuhusu suala hili, kukosekana kwa usawa wa kuwalinda watoto na madhumini ya amri ya kupiga marufuku, wanaweza kuunga mkono zuio hili vyema kabisa- na kura za mara kwa mara zimeonyesha matokeo tofauti sana wakati swali linapoulizwa kwa njia tofauti.

# Mara nyingi nimewasikia vijana wakiongea na kuunga mkono adhabu ya viboko - je tunapaswa kuwasikiliza?

Ni kweli kwamba wakati mwingine watoto watasema kwamba kupewa adhabu za kimwili ni vizuri kwao, kwamba inawafundisha jinsi ya kuwa na nidhamu, au hata kuonyesha kwamba wazazi wao wanawapenda. Na bila shaka tunapaswa kuwasikiliza kile ambacho vijana wanasema. Lakini watu wazima wana wajibu sio tu wa kuwasikiliza bali kuelewa kile ambacho watoto wanatuambia. Tumeanza kuzingatia jinsi ambavyo watoto wanaanza kutuambia kuhusu wanavyoumia kimwili na kihisia baada ya kupigwa (tazama 'Je, ni kweli adhabu za viboko zinaumiza', ukurasa wa 8). Wakati baadhi ya watoto wanasema kuwa hii ni jambo muhimu na ni vizuri, inaonyesha ni jinsi gani walivyokuwa na kuamini kwamba ni jambo la kawaida na ni sawa kuadhibiwa kimwili na wahifadhi imani hii kwenye roho zao, kupokea mitazamo na tabia za wazazi wao na kufikiria au kujaribu kuleta umaana wa maumivu waliyoyapitia.

Watoto wana haki ya msingi ya kuheshimu utu wao wa kibinadamu na uadilifu wa kimwili na usawa wa kulindwa wasipigwe. Ni wajibu wa serikali kuhakikisha kwamba sheria inasimamia haki hizo. Ni wajibu wa wazazi na watu wazima wengine kulea watoto ili wajue haki zao na kuziheshimu kwa ajili yao na wengine

# Kuchapwa nikiwa mtoto hakukunipa madhara yeyote. Ningekuwa hapa nilipo leo ikiwa wazazi wangu wasingeniadhibu kwa viboko?

Hakuna anayejua jinsi tungelivyokuwa kama wazazi wetu wasinge tupiga au kutu aibisha. Na watu wengi, wanaposema kuwa hawakupata madhara yoyote, wanakataa maumivu waliyoyapitia wakati watu wazima waliokuwa karibu nao walidhani njia pekee ya kuwafundisha adabu ni kuwasababishia maumivu.

Watu wazima wanaowapiga watoto wao kwa mgogo wa kuwaadhibu huwa wanaanza kufanya hivyo kwa sababu wao wenyewe pia walikuwa wanapigwa utotoni. Ingawa utafiti unaonyesha mara nyingi huwa wanajihisi kuwa wenye hatia kuhusu suala hilo baadae, wanaendelea kuwapiga watoto wao, hasusani waposhindwa kuwa na uvumilivu. Hakuna faida yoyote ya kulaumu vizazi vilivyopita kwa hili, kwa sababu walikuwa wakifanya kulingana na utamaduni ulioenea wa kipindi hicho. Lakini ni kosa kukataa mabadiliko kwa sababu tunaogopa kuonekana kuwa tunawapinga wazazi wetu. Mambo yanabadilika na jamii inasonga mbele. Kutambua watoto kama wamiliki wa haki ni lazima hatua zichukuliwe za kukomesha uhalali na kitendo cha jamii kukubali unyanyasaji dhidi ya watoto, kama vile jamii ilivyosonga mbele na kukomesha unyanyasaji dhidi ya wanawake.

Watu wengine wanasema: "Nilipigwa kama mtoto na nimekuwa vizuri." Lakini kuna watu ambao wamevumilia kila aina ya uovu wakati wanapokua ambao "wamekuwa sawa" kama watu wazima, lakini hakuna atakayesema kuwa walichokipitia kilikuwa kizuri. Mara nyingi ni jinsi walivyoweza kuvumilia na imewasaidia wao kuwa "sawa", na sio uzoefu wa kupigwa

“Nii kosa **kukataa mabadiliko** kwa sababu tunaogopa kuonekana kuwa tunawapinga wazazi wetu.”

“Adhabu ya kupiga ndio inayotumika zaidi kuwanyanyasa watoto.”

# Kuna aina nyingi ya ukiukaji wa haki za watoto - kwa nini tujikite katika suala hili dogo?

UNICEF imesema kuwa, kuchapa watoto ndio "nidhamu" inayotumika zaidi dhidi ya watoto. Adhabu ya viboko husababisha maelfu ya vifo – hasusani watoto wadogo sana – ulimwenguni kila mwaka na zaidi ya mamilioni wanaumizwa. Sio suala lisilo muhimu au dogo.

Lakini si suala la ulinzi wa watoto tu. Uhalali wa adhabu ya viboko katika nchi nyingi ndio kiashiria cha hali ya chini ya watoto, ambapo wanachukuliwa kama mali na watu wa chini sana badala ya kuchukuliwa kama wamiliki wa haki kamili. Adhabu ya viboko inaonyesha uzoefu wa kila siku wa watoto wengi wa ulimwengu, na katika kila kisa, hadhi ya mtoto na uadilifu wa kimwili hukiukwa. Kama vile kuzuia na kupinga dhuluma ya kinyumbani dhidi ya wanawake kumekuwa jambo muhimu katika uwezeshaji wa wanawake na kukubali haki zao, ndivyo pia ilivyo kwa watoto. Kukataza adhabu ya viboko huongeza hadhi ya watoto na inachangia vyema jinsi wanavyozingatiwa na kutendewa katika jamii. Hakuna serikali inayoweza kujifanya kwamba inawaheshimu watoto kama wamiliki wa haki pamoja na watu wazima, au kujifanya kuwa ina mfumo mzuri na salama wa ulinzi wa watoto wakati sheria yake inasisitiza dhuluma dhidi yao.

5. UNICEF (2014), Hidden in Plain Sight: Uchambuzi wa kitakwimu wa vurugu dhidi ya watoto, NY: UNICEF.

# Wazazi wana haki ya kulea watoto wao kadiri wanavyoona inafaa. Je, hawapaswi kupingwa tu katika hali mbaya za unyanyasaji wa watoto?

SoJamii zimeacha kuona watoto kama mali ya wazazi wao na kuwaona kama watu katika haki yao wenyewe. Kama binadamu, watoto hufurahia haki za kibinadamu – lakini huwa hawazipati. Watoto wana haki sawa na wanafamilia wengine ya kulindwa kutokana na kupigwa, na sio uvamizi tena wa faragha na maisha ya kifamilia kusisitiza kwamba sheria inalinda watoto dhidi ya kushambuliwa nyumbani kuliko kusisitiza kwamba inawalinda watu wazima dhidi ya dhuluma za wapenzi wa karibu.

Makubaliano ya UN kuhusu Haki za Mtoto yanahimiza umuhimu wa familia na inakuza dhana ya uwajibikaji wa wazazi, na masilahi bora ya watoto kama maswala msingi ya wazazi (kifungu cha 18). Watu wengine wanasema, kwa kinyume, kwamba kumpiga mtoto kwa jina la nidhamu, kwa kweli, ni kwa faida ya mtoto kwa muda mrefu. Lakini kama Kamati ya Haki za Mtoto imesema:[6]

"...Tafsiri ya masilahi mazuri ya mtoto lazima iambatane na Mkutano wote, ikijumuisha jukumu la kulinda watoto kutokana na kila aina ya dhuluma na hitaji la kutoa uzito unaofaa kwa maoni ya mtoto; haiwezi kutumiwa kuhalalisha mazoea, ikijumuisha adhabu ya viboko na aina nyingine za adhabu kali au yenye kudhalilisha, ambayo inapingana na hadhi ya binadamu na haki ya uadilifu wa kimwili."

Mwishowe, wazazi pia wanastahili kufaidika kutokana na ujumbe wazi kwamba adhabu ya inayodhulumu inahusishwa na uhusiano duni wa kifamilia na orodha ndefu ya matokeo hasi kwa watoto wao, bila viungo vya matokeo yoyote mazuri.

6. Maoni ya jumla namba 8 ya mwaka (2006) juu ya "Haki ya mtoto ya kulindwa dhidi ya adhabu ya kichapo na aina nyingine ya ukatili au adhabu za kushusha hadhi (fani. 19; 28, aya. S2; and 37, inter alia)", para. 26, inapatikana kwenye: endcorporalpunishment.org/wp-content/uploads/key-docs/CRC-general-comment-8.pdf.

# Kuna tofauti kubwa kati ya kumpiga mtoto na kumpa kofi la upendo. Je, kuzuia adhabu ya viboko siyo kuchukua hatua ya mbali mno?

Kumpiga mtoto kunaweza kumuumiza zaidi kuliko "kofi la upendo" (lakini angalia 'Je, adhabu ya viboko si inaumiza sana', ukurasa wa 8), lakini zote mbili ziko kwenye mwendelezo wa dhuluma na zote zinakiuka haki ya mtoto ya kuheshimu hadhi ya kibinadamu na uadilifu wa kimwili. Jamii hazitoi viwango wala hazijaribu kuhalalisha kiwango chochote cha dhuluma wakati zinaongelelea dhuluma dhidi ya wazee. Kwa hivyo ni kwa nini wanapaswa kuweka viwango kwa watoto? Na hatari ya kufanya muunganisho wowote kati ya kupenda na kuumiza watu zinapaswa kuwa wazi. "Kumpiga mtoto ili kumrudi" ni utata wa aina mbaya zaidi. Neno hili linalonekana kuwa halina madhara ni pazia ambapo ukiukaji wa haki unaweza kujificha.


Watu wengine wanasema kuwa "kuna tofauti kubwa kati ya unyanyasaji wa watoto na kofi jepesi", kwa kuzingatia kidogo nia ya "kupenda" kuhusu dhuluma na zaidi kuhusu kiwango cha dhuluma inayotumika. Hata hivyo, sio sahihi kupendekeza kwamba watu wazima wawe na udhibiti sahihi kuhusu kiwango cha unyanyasaji wanachotumia. Utafiti unaonyesha kwamba mara nyingi nguvu nyingi hutumiwa kuliko inavyokusudiwa,[7] na kwamba kiwango

7. Kirwaun, S. & Bassett, C. (2008), Uwasilishaji kwa NSPCC: Adhabu ya viboko, Ofisi ya Utafiti wa Masoko Uingereza/Jumuiya ya Taifa ya Kuzuia Ukatili kwa Watoto.

8. Shergill, S. S. et al (2003), "Two eyes for an eye: The neuroscience of force escalation", Science, vol. 301, 11 July 2003, p. 187.

cha kutumia nguvu huongezeka.[8] Na tena, kupiga mtoto kwa ukali wowote, kunakiuka haki ya mtoto ya kuheshimu uadilifu wake wa kimwili.

Watunga sheria na serikali wametenganisha "unyanyasaji wa watoto" na "adhabu ya kiboko" kwa njia ya kijadi, lakini unyanyasaji mwingi ni adhabu ya kiboko – watu wazima wanawashambulia watoto ili kuwaadhibu na kupata udhibiti. Hakuna kizingiti kama hicho kinachopendekezwa katika kesi ya dhuluma dhidi ya wazee, ambapo uvumilivu usiokuwepo unaonyesha wazi ujumbe kwamba unyanyasaji wowote haukubaliki. Lakini kwa watoto, watu wazima wameunda tofauti ya kihalali kati ya dhuluma ya adhabu ambayo inakubalika, na "dhuluma" ambayo haifai. Kwa kweli, haiwezekani kutofautisha kati ya dhuluma ya watoto na adhabu ya viboko.





# “Hakuna kitu kama kofi ‘salama’.”

# Kwa nini tusifafanue kofi salama, badala ya kukataza yote?

Hakuna kitu kama kofi "salama". Kupigana kwokote huingilia kati uadilifu wa mtoto wa kimwili na huonyesha kutokuheshimu hadhi yao ya kibinadamu. Utafiti mwingi umeonyesha aina zisizo kali sana za adhabu ya viboko inayofanywa na wazazi kuwa hatari ya dhuluma kali inayochukuliwa kama unyanyasaji, na tabia ya kuongezeka na kutokuwa sahihi katika kujua kiwango cha nguvu inayotumika tayari imejadiliwa (angalia 'Kuna tofauti kubwa kati ya kumpiga mtoto na kumpiga ili kumrudi. Je, si kuzuia adhabu ya kiboko inapeleka vitu mbali sana? ' ukurasa wa 20).

Nchi chache zimejaribu kufafanua njia zinazokubalika za kupiga watoto – katika umri gani, katika sehemu gani za mwili kwa kutumia vifaa gani na kadhalika. Pamoja na kutuma ujumbe usiojulikana sana kuhusu mtazamo wa jamii kuhusu unyanyasaji kwa watoto, hili ni zoezi lisiloweza kutolewa. Hatutafikiria kujaribu kufafanua njia zinazokubalika za kushambulia wanawake au wazee au kikundi chochote cha watu. Watoto wana haki sawa ya ulinzi dhidi ya kushambuliwa. Ikiwa kuna chochote, watoto – kwa ujumla ni wadogo na wadhaifu zaidi kuliko sisi wengine – wana haki ya kulindwa zaidi.

# Dini yangu inaniruhusu nitumie adhabu ya viboko. Je, haitakuwa ubaguzi kunikataza kutumia adhabu hiyo?

Kupiga watoto hakuendani na maoni, maadili na imani za dini kuu za ulimwengu, ambazo zinadai huruma, usawa, haki na bila dhuluma. Wafuasi wa dini za ulimwengu wanaiga maisha yao kwa mfano na mafundisho ya waanzilishi wao. Wasomi na wanatheolojia wanasisitiza kwamba hakuna ushahidi wowote uliorekodiwa wa waanzilishi wa dini kuu kuhusu kumpiga mtoto.

Mtazamo wa kidini ambao unaruhusu adhabu ya viboko kwa watoto mara nyingi unatokana na utamaduni wa kiimla, nguvu na udhibiti wa watoto. Inahusu utii potofu kama wema na unyanyasaji wa kupiga mtoto kama jibu linalokubalika kwa watoto wanaosemekana kutokuwa na adabu.

Viongozi wa kidini ni baadhi ya waharakati wa kidunia wa kokumesha adhabu ya viboko kwa watoto. Zaidi ya viongozi 800 wa kidini wakiwa katika mkutano wa dini na amani mjini Kyoto, Japan (2006) walisaini azimio – Makubaliano ya kidini ya kupiga vita unyanyasaji wa watoto (Mkataba wa Kyoto) ambao unahamasisha serikali kuunda sheria za kusitisha unyanyasaji wa aina yeyote ikiwa ni pamoja na kukomesha adhabu ya viboko kwa watoto.[9]

9. Maelezo yote kuhusu azimio hili yanapatikana kwenye: http://churchesfornon-violence.org/wp/wp-content/uploads/2012/02/Violence-Against-Children-3.pdf.

Kamati ya Haki za Watoto, katika Nukuu yake nambari 8 inasisitiza kwamba haki za kidini zina mipaka ambayo imewekwa ili kulinda haki na uhuru wa wananchi wengine.[10] Kamati inaeleza:[11]

"Baadhi ya sababu za kidini zilizotolewa kuhalalisha adhabu ya viboko, zikipendekeza kwamba ufasiri fulani kuhusu maandishi ya kididni zinatetea umuhimu wa kutumia adhabu hiyo. Uhuru wa kidini ni thibitisho kwa kila mmoja katika Mkataba wa kimataifa wa haki za kiraia na kisiasa (ibara ya 18), lakini mafunzo ya kidini au ya imani yawe sambamba na heshima na ubinadamu kwa watu wote...."



10. Maoni ya Jumla Nambari 8, aya. 29.
11. Maoni ya Jumla Nambari 8, aya. 29.

# Je, kwa nini tunaingiza sheria katika suala hili? Kwa nini wazazi wasielimishwe tu kuacha kutumia adhabu ya viboko?

Kupigwa marufuku kwa adhabu ya viboko na adhabu nyingine mbaya zenye kudhalilisha kunahitaji elimu na kusitishwa. Hili sio suala la mjadala. Haki za binadamu zinasisitiza kwamba watoto na watu wazima wana haki sambamba zinazowalinda – katika familia na mahali kote. Sheria yenyewe ni chombo cha elimu chenye sauti kubwa, na kurekebishwa kwa sheria inayopiga marufuku adhabu ya viboko kunahitaji kuunganishwa kwa umma na elimu kwa wazazi. Sheria itawahimiza wazazi kuangalia njia halisi za kuwalea watoto wao na kuwatia moyo wataalamu, wanasiasa, na pia vyombo vya habari katika kutoa elimu kuhusu njia hizo.

Kuna utata na ugumu katika kuelimisha wazazi kuacha hatua ambayo inaungwa mkono na sheria. Kinachochukuliwa ni kwamba, kama sheria inaruhusu adhabu hiyo basi sio vibaya kuitumia. Elimu inaufanisi zaidi ikiwa sheria inatoa maoni yanayoenda sambamba na elimu hiyo.

# Adhabu ya viboko inatolewa na familia majumbani na si hadharani; itakuwa vigumu kuiwekea sheria, kwa hiyo kuna sababu gani ya kuisitisha?

Hakuna mtu siku hizi ambaye anashauri kuacha unyanyasaji wa watu wazima katika familia kwa sababu ni vigumu kuwaadhibu: Kwa nini hakuna sheria kamilifu ya kuwalinda watoto? Sababu ya kwanza ya kurekebisha sheria ya kukomesha adhabu ya viboko ni kinga – kuwakinga watoto na mashambulio yanayoumiza kabla hayajawatokea. Hii ni nia ya kwanza ya sheria madhubuti: Kuweka kanuni na kutoa ujumbe unaoeleweka, ukiwa ni pamoja na kuzingatia hatua hii majumbani. Lakini kusitishwa kwa adhabu hii kunatakiwa kuidhinishwa kwa uangalifu, hii ni kwa sababu ya kuwasaidia watoto – kwa vile kama adhabu ya viboko ikithibitishwa kuwa ni kosa, hakutasababisha wazazi kuhukumiwa na watoto kutunzwa katika vituo vya watoto?' ukurasa wa 40.

Kuanzisha usitishaji unatakiwa kufuatana na kampeni madhubuti zinazotoa maelezo na kuelekeza wazazi katika kuchukua hatua ya kulea watoto bila kuwanyanyasa.

# Je, hatuwezi kusubiri hali za wazazi za kila siku kuboreka kabla ya kusitisha adhabu ya viboko, ili swala hilo lisiwaongezee matatizo zaidi?

Ubishi huu ni uafiki wa kweli ulio wazi: Kwa mara nyingi adhabu ya viboko inatolewa pale watu wazima wanapotaka kutoa hasira mioyoni mwao na sio kama kigezo cha kuwalea watoto. Katika nyumba na vyuo vingi, watu wazima wanahitaji msaada na vielelzo zaidi, hata ikiwa matatizo ya watu wazima yakiwa makubwa iliyoje, kuwekea watoto hasira haikubaliki. Ulinzi wa watoto hauhitaji kusubiri maisha ya watu wazima kuboreka, kama ambavyo unyanyasaji wa wanawake kusivyoweza kungoja hali za wanaume kuboreka.

Kwa vyovyote vile, kuwapiga watoto hakusaidii kuondoa mfadhaiko. Watu wakubwa ambao huwapiga watoto kwa hasira husikia hatia; wale wanaopiga bila ya kujali hisia hugundua kuwa wanakabiliana na watoto wenye uchungu na hasira. Maisha katika majumba na vyuo ambapo adhabu ya viboko haitumiki yamekua yakionyesha nidhamu na hali nzuri kwa wote.

Katika nchi zilizokabiliwa na vita, watu wanaofanya kazi na watoto, wakiwemo wazazi na walimu, ni wale waliopitia unyanyasaji na udhalilishaji. Wanakubaliana na kulinda haki za watoto, lakini wanafikiria nani anayetetea haki zao. Haya makandamizo ya haki yanatakiwa yafuatiliwe lakini watoto wanatakiwa wasingoje hadi watu wakubwa waweze kufurahia haki zao. Watu wote wana haki ya kuheshimu hadhi na uadilifu wao na pia ulinzi sawa chini ya sheria-watoto ni watu pia.



"Watoto duniani kote, **wana haki** ya kuishi maisha yasiyo na vurugu ya aina yoyote."

# Swala hili linamsingi wake kwa weupe, Ulaya. Adhabu ya viboko ni sehemu ya utamaduni wangu na mazoea ya malezi ya watoto. Je, si ubaguzi kupiga marufuku sheria hii?

Wazo la kwamba kupiga watoto ni desturi ya kujivunia halikubaliki. Katika tukio lolote lile, upigaji wa watoto unaelekea kuwa desturi ya watu weupe, ulioenezwa katika pande nyingi za dunia kwa njia ya utumwa na ukoloni na pia kwa elimu kupitia kwa wamishionari. Katika utetezi wa kiingereza wa " sababu kuu " kwa mfano, umejitokeza katika sheria zote duniani. Inaonekana kwamba tamaduni ambazo zinatoa adhabu kidogo au hazina adhabu kwa watoto ni zile zenye watu wachache, jamii za wawindaji, watu wenye asili za kale kati ya wote, ingawa asili hiyo inaendelea kupotea kwa kasi sababu ya kustaarabika kwa miji na utandawazi.

Lakini haki za binadamu ni za ulimwenguni, na watoto duniani kote wana haki ya kuishi maisha yasiyo na vurugu. Tamaduni zote zina jukumu la kukana adhabu ya viboko, kama zilivyokana maswala mengine ya haki za binadamu ambayo yameunda sehemu ya desturi zao. Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watoto unadumisha haki zote za watoto kuwakinga kutokana na aina zote za unyanyasaji wa kimwili na kiakili, bila ya kubagua, kabila, tamaduni, desturi na dini. Kuna uhamasisho wa kupiga marufuku kwa adhabu ya viboko kwa watoto katika nchi zote barani. Mapigo yanayofanyika mashuleni na katika vyombo vya sheria yameharamishwa katika kanda zote duniani.

# Je, kwa nini ni vigumu kuacha kupiga watoto?

Ikiwa watu wazima, ikiwemo wanasiasa, wameona urahisi wa suala hili, tungeshakubali tangu mwanzo kwamba watoto wana haki sawa na wote kuheshimu utu wao kama binadamu na ulinzi sawa chini ya sheria. Kwa kweli, tutakuwa tunakubali kwamba watoto ambao wanaanza wakiwa wadogo na dhaifu, wana haki ya kulindwa zaidi kuliko watu wazima.

Inaonekana kuna sababu nyingi ambazo zinafanya iwe vigumu kwa wazazi kuachana na kile ambacho bado wanakichukulia kama "haki" ya kuwapiga na kuwaumiza watoto kwa ajili ya "nidhamu" au udhibiti:

(i) Uzoefu binafsi. Kila mahali watu wengi walipigwa na wazazi wao wakati walipokuwa watoto. Wazazi wengi wamewapiga watoto wao. Hakuna hata mmoja kati yetu anayependa kuwafikiria vibaya wazazi wetu au malezi yetu wenyewe, na hili linaleta changamoto kwa watu wengi wakiwemo wanasiasa na watu mashuhuri na hata wale wanaofanya kazi za kumlinda mtoto, kuchukulia adhabu ya viboko kama jambo la msingi la usawa na haki za kipinadamu kama lilivyo. Hili sio suala la lawama-wazazi walifanya hivyo kulingana na matarajio ya jamii-lakini sasa muda umefika wa kuanza mahusuiano mazuri na yasiyo na vurugu kwa watoto.



(ii) Watu wazima huwapiga watoto mara kwa mara kwa sababu wana hasira, au msongo wa mawazo, au wamefikia ukomo wa uvumilivu. Watu wazima wengi wanatambua, ndani ya mioyo yao, kwamba kupiga ni itikio la kihisia na sio maamuzi ya kimantiki ya kumfundisha "nidhamu" mtoto. Inavyozidi kutokea mara nyingi, ndivyo kupiga mtoto kunakuwa ni njia ya mazoea ya kushughulikia wenye tabia mbaya au sumbufu. Sio rahisi kubadili tabia za kimazoea. Lakini zinaweza kubadilishwa. Kwa kuwa serikali inawekeza kwenye elimu ya umma na uhamasishaji kuhusu njia chanya na sisizo za vurugu za kuwalea watoto na kuhusu haki za watoto kuheshimu hadhi yao na uadilifu wa mwili, wazazi wataanzisha njia mbalimbali za kushughulikia tabia ambazo hawazitaki bila kuhisi uhitaji wa kuwaumiza watoto wao.

(iii) Ukosefu wa elimu kuhusu njia mbadala. Mabadiliko ya sheria lazima yaambatane na elimu ya wazazi, watoto na jamii kwa ujumla kuhusi uwepo wa njia nyingi chanya sisizotumia vurugu ambazo watu wazima wanaweza kuzitumia kwa watoto.



# Sehemu ya 2: Maswali kuhusu athari ya kuzuia adhabu zote za viboko



# Kama wazazi watalazimishwa kuachana na adhabu ya viboko, watoto hawataharibika na kukosa nidhamu?

Hapana! Nidhamu sio sawa na adhabu. Adabu halali haitumii vurugu. Inajengeka kutokana na maafikiano, kuheshimiana, stahamala na mawasiliano bora ya pande zote mbili. Watoto wachanga wanaanza wakiwa wategemezi, na wanavyokua, huwategemea watu wazima -hususan wazazi wao- kuwaongoza na kuwasaidia kuelekea ukomavu binafsi wa kinidhamu. Adhabu ya viboko haimwambii mtoto chochote kuhusu namna anavyopaswa kujiheshimu au kushika adabu. Kinyume chake, kuwapiga watoto ni fundisho kwa tabia mbaya. Kunawafundisha watoto kwamba wazazi wao wanaona ni sahihi kutumia vurugu kutatua matatizo au migogoro.

Kuwapiga watoto pia kunatoa ujumbe tatanishi kwa watoto kwamba ingawaje hawapaswi kuwapiga watoto wengine au watu wazima na watu wazima kutokuwapiga watu wazima wengine, ni sahihi kwa watu wazima ambao ni wakubwa na wenye nguvu, kuwapiga watoto ambao ni wadogo na wanaoweza kudhuriwa. Watoto wanajifunza kutoka kwa matendo ya wazazi wao, na sio wanayoyasema tu.

Na heshima isichanganywe na uoga. Tabia "bora" kwa kuhofia kuadhibiwa inamaanisha kwamba mtoto anaepuka adhabu na sio kuonyesha heshima. Watoto hujifunza kuheshimu watu na vitu kwa dhati wakati wanafurahia thamani yao ya ndani. Wazazi wakiwapiga watoto wao kwa kisingizio cha nidhamu, watoto wanajifunza "kushika adabu" kwa lengo la kuepuka adhabu, na wanajifunza kwamba kutumia vurugu ni njia sahihi ya kushughulikia ugomvi. Lakini wazazi wakionyesha heshima kwa utu na uadilifu wa watoto wao na watu wengine, watoto wanajifunza kuhusu heshima. Wazazi wakiwaadhibu watoto wao kwa kutumia njia chanya na sisizo na vurugu, watoto hujifunza kwamba mzozo unaweza kutatuliwa bila kudhalilisha heshima hii.

Adhabu ya viboko na nyingine za kikatili na kuvunja heshima sio mbadala wa njia nzuri za nidhamu au adhabu. Mbali na kuwaharibu watoto, adhabu dhahiri imeundwa kuhakikisha kuwa watoto wanajifunza kuwafikiria wengine na matokeo ya matendo yao. Nchi zina wajibu wa kuunga mkono malezi mazuri. Kuna mambo mengi yanayohamasisha malezi chanya na elimu bila kutumia vurugu, ambayo yanaweza kutoholewa na kufasiriwa kwa matumizi ya kila nchi.



# Endapo adhabu ya viboko itapigwa marufuku, je kitendo hiki hakitapelekea watoto kuadhibiwa kwa njia za kutisha zaidi- unyanyasaji wa kihisia, udhalilishaji na kufungwa?


Watoto wana haki ya kulindwa dhidi ya adhabu ya kutandikwa na aina nyingine zote za adhabu za kikatili, kuvunjiwa heshima na kunyanyaswa. Mabadiliko ya sheria yanafaa kuhusishwa na utoaji wa elimu na uhamasishaji wa mahusiano mazuri na yasiotumia vurugu kwa watoto. Wazazi wanataka watoto wao wawe na mwanzo mzuri na bora kwenye maisha.

Wazazi wanaowapiga au kuwatendea vibaya watoto wao kwa upande mwingine huhisi vibaya kuhusu vitendo hivyo- Kiujumla, wanafadhaika na kujihisi wenye hatia au makosa. Wazazi wengi wangepokea ushauri na msaada wa jinsi ya kuzuia na kutatua migogoro dhidi ya watoto wao bila kutumia aina yeyote ya vurugu, kimwili au kihisia. Kuacha kuwapiga na kuwadhalilisha watoto na kuanza kuwatazama kama watu na wenye haki kama sisi, huboresha maisha ya kifamilia na ya kila mtu.

# Kama adhabu ya viboko ikafanywa kuwa kosa la jinai, maelfu ya wazazi hawatashtakiwa na watoto wengi kuwekwa chini ya uangalizi?

Dhumuni la sheria kupiga marufuku adhabu ya viboko sio kuwaweka wazazi zaidi gerezani. Inahusu kutimiza haki za watoto na kuibadilisha jamii kuelekea kwa mahusiano mazuri na yasiyotumia vurugu kwa watoto. Hakuna ushahidi wa ongezeko la kushtakiwa kwa wazazi kutoka kwenye ongezeko la nchi ambazo adhabu ya kutandikwa ni kosa la jinai.

Kupiga marufuku adhabu ya kutandikwa kunatimiza masharti ya nchi ya haki za binadamu kwa watoto. Lengo lake la kwanza ni la kielimu-Kupeleka ujumbe wa wazi majumbani kwamba haikubaliki tena na sio jambo la kisheria kumpiga mtoto kuliko kumpiga mtu mwingine yeyote. Mwongozo kwa wote wanaohusika na ulinzi wa mtoto wakiwemo polisi na mamlaka za sheria, lazima uhakikishe kwamba utekelezaji wa sheria unalenga maslahi ya mtoto. Mashtaka na taratibu nyingine maalumu za uingiliaji kati haziwezi kuwanufaisha watoto mpaka pale zitakapokuwa njia pekee za kufanikisha ulinzi wa watoto kutoka kwenye madhara makubwa.



Kwenye maoni yake ya jumla Namba 8, Kamati ya haki za watoto imeeleza kanuni mbili ambazo zitahakikisha kwamba kuharamishwa kwake hakusababishi kuongezeka kwa kushtakiwa kwa wazazi:

1. Kanuni ya de minimis – inamaanisha kuwa sheria haifai kujihusisha kwa mambo ya kipuuzi, na ndiyo maana mara nyingi, mizozo midogo kati ya watu wazima huwa haisuluhishwi mahakamani. Kanuni iyo hiyo inaweza kutumika pale watu wazima wanapowaumiza kidogo watoto.

2. Kwa sababu watoto huwa wategemezi na upendo wa pekee unaotokana na mahusiano ya kifamilia, uamuzi wa kuwashtaki wazazi au kuingilia kati masuala ya kifamilia unafaa kufanywa kwa umakini mkubwa na kufanywa wakati inabidi ili kuwalinda watoto kutoka hatari kubwa na kwa manufaa ya mtoto.

# Kwani kuna tatizo wazazi kuwapiga watoto wao makofi ili kuwazuia kujiumiza?

Kuwapiga watoto makofi ili kuwazuia kujiumiza hakuna mantinki yoyote! Unaweza kufikiri kuwashauri wazazi kwamba watoto wao wanapokuwa hatarini, wanalazimika kuwapiga? Bila shaka, hapana.

Wazazi wanalazimika kutumia matendo halisi/wazi kuwalinda watoto – hasa watoto wachanga na wadogo – kila wakati. Ni sehemu ya asili ya malezi. Ikiwa mtoto anatambaa kuelekea kwenye moto, au kukimbia kuelekea kwenye barabara hatari, kikawaida, wazazi hutumia nguvu kuwazuia – kwa kuwashika, kuwabeba, na kuwaonyesha na kuwaambia kuhusu hatari. Lakini kuwasababishia maumivu kwa kuwapiga inapoteza ujumbe kwamba wanalazimika kuhakikisha kuwa wanakuwa salama na kuwa, hadi watakapoweza kufanya hivyo, wazazi wao watahakikisha wako salama. Kama Kamati ya Haki za Mtoto inavyoeleza:[12]

"... kulea na kuwatunza watoto, hasa watoto wachanga na wadogo, huhitaji matendo halisi na uingiliaji kati wa mara kwa mara ili kuwalinda. Hili ni tofauti na maamuzi ya makusudi na adhabu zinazotumia nguvu ili kumsababishia mtoto maumivu kwa kiwango fulani, kero/ adha au udhalilishaji. Kama watu wazima, tunajua tofauti kati ya kuchukua hatua ili kuwalinda na adhabu zinazowaumiza; si vigumu kujua tofauti kati ya mambo yanayowahusu watoto."

12. Maoni ya Jumla Nambari 8, aya. 14.

Kuna utofauti mkubwa baina ya kutumia nguvu kuwalinda watoto na kuwaadhibu kwa lengo la kuwaumiza. Sheria za nchi ziko wazi, zinaruhusu adhabu mbadala zisizo na madahara  kuwalinda watu. Kuondoa haki ya kutumia nguvu katika kuadhibu haiingilii hii kabisa.



# Tovuti ya Global Initiative:

**www.endcorporalpunishment.org**

Kuna maelezo mapana kuhusu vipengele vyote vya kuzuia adhabu ya viboko kwenye tovuti ya Global Initiative, ikiwa ni pamoja na:

- Ripoti zenye maelezo ya kina kuhusu kila jimbo na maeneo yote ulimwenguni.
- Majedwali ya ulimwengu na kanda yanayoeleza maswala ya sheria kuhusu adhabu ya viboko na fursa za kufikia mabadiliko ya kisheria.
- Jinsi Umoja wa Mataifa na mifumo ya kikanda ya haki za binadamu yanavyoshughulikia adhabu ya viboko, na maelekezo kuhusu jinsi ya kutumia mbinu hizi ili kuhamasisha mabadiliko ya kisheria.
- Maelezo mafupi ya tafiti kuhusu kuenea na hisia za watu kuhusu adhabu ya viboko, na athari ya adhabu ya viboko kwa watoto, watu wazima na jamii.
- Taarifa kuhusu kuunga mkono kutekelezwa kwa upigwaji marufuku.
- Rasilimali tetezi za kimataifa na kikanda, zikiwemo rasilimali zilizo kwa lugha nyingi tofauti.



# Wakati wa kukomesha adhabu ya viboko kwa watoto umefika. Sasa watoto wana haki ya kuheshimiwa na kulindwa kutoka kwa aina zote za unyanyasaji!

**Mpango wa Kukomesha Adhabu zote za Viboko kwa Watoto Duniani**
(Global Initiative to End All Corporal Punishment of Children)

Mpango wa Kukomesha Adhabu zote za Viboko kwa Watoto Ulimwenguni unaendeleza uzuiaji na kukomesha adhabu za viboko na kutoa msaada wa kiufundi na ushauri wa bure kuhusu mageuzi ya vipengele vyote vya sheria.

*www.endcorporalpunishment.org*

*info@endcorporalpunishment.org*

*www.twitter.com/Glendcorpun*

*www.facebook.com/Glendcorporalpunishment*

**Shirika la Save the Children Sweden**

Shirika la Save the Children Sweden linaunga mkono kuzuiwa kwa adhabu za viboko katika mazingira yote. Mnamo mwaka 1979, shirika la Save the Children lilichangia kuifanya Sweden kuwa nchi ya kwanza ulimwenguni kupiga marufuku adhabu za viboko kwa uwazi. Shirika la Save the Children linashughulika kufanikisha marufuku ya kisheria na kukomeshwa kwa adhabu za viboko na kufanya suala hili kuwa ajenda ya kisiasa ulimwenguni kote.

*info@rb.se*

*www.raddabarnen.se*

*resourcecentre.savethechildren.net*

GLOBAL INITIATIVE TO
End All Corporal
Punishment of Children

Save the Children